# OFISI YA RAISI –TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

**SHULE YA SEKONDARI KYANG'OMBE,**
**S L P 31,**
**MUSOMA.**
**………………………………**

**KUMB NA. KSS/HWR/JI/2024/……..**

**JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………………………………………………………..**
**S L P ……………………………………………………………..**
**………………………………………………………………**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KYANG'OMBE MWAKA 2024**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza** katika shule ya sekondari Kyang'ombe mwaka 2024. Hongera sana kwa kupata hiyo.
Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **08/01/2024.** . Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **08/01/2024** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **15/01/2024.**

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 Sare ya shule**

**WAVULANA.**

i. Suruali mbili (02), moja ya rangi ya khaki na nyingine ya rangi nyeusi, yenye marinda mawili upande wa kulia na kushoto, chini ziwe na upana usiopungua nchi 18 na ziwe na turnup (**modal haziruhusiwi**)
ii. Sweta yenye kola ya V rangi ya blue
iii. Shati mbili nyeupe za mikono mifupi zisizobana mwili
iv. Tai mbili, moja nyeusi na nyingine ya khaki
v. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kamba , vyenye visigino vifupi.
vi. Soksi nyeusi.
vii. Tisheti ya kola yenye nembo ya shule (utapewa utaratibu wa kuipata utakaporipoti),
viii. Bukta ya rangi ya bluu na track suit nyeusi yenye mchirizi mweupe kwa ajili ya michezo
ix. Raba za michezo
x. Mkanda mweusi wa ngozi.

**WASICHANA.**

i. Sketi mbili (02) kitambaa kizito moja ya rangi ya **khaki** na ya pili rangi nyeusi, zenye fito (michirizi) mbili nyeupe na marinda ya kawaida. Ziwe ndefu zifike kwenye kifundo cha mguu.
ii. Sweta yenye kola ya V rangi ya blue

iii. Shati mbili nyeupe za mikono mifupi zisizobana mwili. Rangi ya Hijabu iwe nyeupe.
iv. Tai mbili, moja nyeusi na ya khaki
v. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kamba , vyenye visigino vifupi.
vi. Soksi ndefu (stockings) nyeupe.
vii. Tisheti ya kola yenye nembo ya shule (utapewa utaratibu wa kuipata utakaporipoti)
viii. Track suit nyeusi yenye mchirizi mweupe kwa ajili ya michezo
ix. Raba za michezo

**2.2 Daftari kubwa (counter book quire 2) 09 na madaftari madogo 06 , kalamu, rula, penseli na mkebe wa hesabu.**
**2.3 English to English Dictionary**
**2.4 File folder moja ya rangi ya khaki na kamba yake**
**2.5 Ream moja (1) aina ya DOUBLE A**
**2.6 Nakala ya Cheti cha kuzaliwa**

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu **Na 25** ya **mwaka 1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na .10** ya **mwaka 1995 .** Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi , yenye dhamana na elimu nchini na Ofisi ya Rais -**TAMISEMI** yenye jukumu la Usimamizi na uendeshaji Elimu .
Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni

a) Heshima kwa viongozi , wazazi , wafanyakazi wote , wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima:
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation );
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii ;
f) Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule ;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote ; na
h) Kutunza mali za umma

### 3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi , cocaine, mirungi, kuberi, na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito /kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba

k) Kugoma ,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) kuwa na simu ya mkononi

**3.2 MAMBO AMBAYO MWANAFUZI HARUHUSIWI KUFANYA AKIWA SHULENI:-**

a) Kuvuta sigara
b) Kufuga kucha ndefu na nywele ndefu
c) Kufuga ndevu
d) Kuvaa mavazi yasiyo sare rasmi ya shule
e) Kugombana
f) Kuiga mitindo ya kihuni isiyofaa kama vile kuvaa kata – K, kunyoa kipara , kupaka kucha rangi n. k
g) Kuchubua ngozi ya mwili kwa kutumia madawa
h) Kwenda nje ya shule bila ruhusa
i) Kuvaa kofia , bangili, na mapambo mengine yoyote
j) Kuwa na simu , Kamera na Redio shuleni
k) Kukiuka RATIBA au UTARATIBU wa shule
l) Kwenda kwenye nyumba za Walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa/sababu ya muhimu.
m) Kula darasani.
n) Kutotii agizo /maelekezo ya viongozi /walezi.
o) Kwenda kwenye kumbi za starehe, miziki n.k

**4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

**a)** Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni .
**b)** Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo , fujo na makosa ya jinai.
**c)** Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatayotolewa na shule .

**Tafadhali soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu na siku ya kuripoti shuleni mwanafunzi aje na mzazi/mlezi na sio aje peke yake.**

**KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KYANG'OMBE**

……………………………………………………………

**URASA M. MWANGA**
**MKUU WA SHULE**
**0752062190**

**HISTORIA/TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Jina la Ukoo ………………….Jina la kwanza …………..… Jina la Kati …………….
2. Jina la Mzazi/Mlezi ……………………………  Namba ya simu……………..……
3. Kama ni Mlezi: Uhusiano ……………………….…. ………..
4. Anwani ya Kudumu ya Mzazi/Mlezi ……………………………….…….….…
5. Mahali mwanafunzi alipozaliwa: MtaaWa/Kijiji cha ……………..…. Kata ya ………..

   Wilaya ya ……………………………………….Mkoawa ……………………………
6. Dini …………………………….…….. Dhehebu ……………………..…………
7. Unaingia Kidato cha ……………………..……. Tarehe/Mwaka ……………….………
8. Kutoka shule ya msingi …………………… Wilaya …………..… Mkoa ………
9. Mzazi/mlezi wako anafanyakazi ya …………………Mahali ………
10. Kabla hujaja hapa shuleni umepimwa na daktari? Ndiyo/Hapana.
11. Ni ugonjwa/tatizo  lipi ni la kudumu kwako? …………………….………………
12. Sifa maalumu kama unazo/yo…………………………….…………………….
13. Taarifa za Wazazi wako: Wapo hai (….) Wamefariki (……)  (Weka tiki panapohusika).

Nakiri kuwa maelezo yaliopo hapo juu ni sahihi.

**…………………………………**                                        **…………………….…….**

**JINA NA SAINI YA MWANAFUNZI**                                **JINA NA SAINI YA MZAZI/MLEZI**

**KIAPO (HATI) YA KUKUBALI KANUNI, SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE**

**A: KIAPO CHA MWANAFUNZI.**

Mimi (jina la Mwanafunzi) …………………………………………..nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa  na Taifa ya kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Kyang'ombe.

Naahidi kufuata **Kanuni Na Sheria** zilizotajwa hapo juu pamoja na sheria zote na tararibu zote zitakazotolewa na Uongozi wa Shule ikiwemo kuhudhuria shuleni siku zote. Na endapo nitafanya kinyume na **Kanuni na Sheria** hizo nichukuliwe hatua mara moja**.**

**Saini ya Mwanafunzi………………………………………**          **Tarehe……………….**

**B: KIAPO CHA MZAZI / MLEZI**

Mimi (Jina la mzazi /mlezi)……………………………………….ambaye ni Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi…………………………………….  nimeyasoma masharti na sheria zote za shule ya Sekondari Kyang'ombe, naahidi ya kwamba nitamuhimiza mwanangu kufuata sheria nataratibu zote za shule ikiwemo kuhudhuria shuleni siku zote.  Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia bora na mwema wa Taifa letu. Pia naahidi kumkamilishia mahitaji yote ya shule. Na nitakaposhindwa kuwajibika ipasavyo hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

**Saini ya Mzazi/ Mlezi……………………..**                    **Tarehe……………….**

**THE PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**KYANG'OMBE SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

***(To be filled by an Authorized Government Medical Officer)***

Full name of Student …………………………………………………………………. Age ……………………

Height (in cms) …………………………………… Weight (in kgs) ……………………………………..

1. Blood Count ( Red and White)…………………………………………………………………………………
2. Stool Examination………………………………………………………………………………………………
3. Urine Analysis……………………………………………………………………………………………………
4. Syphilis and other V .D …………………………………………………………………………………………
5. T .B and Leprosy Test …………………………………………………………………………………………
6. Eye Test ……………………………………………………………………………………………………………
7. Ears Test …………………………………………………………………………………………………………
8. Chest Test…………………………………………………………………………………………………………..
9. Abdominal Test ………………………………………………………………………………………………
10. Pregnancy Test (Girl)……………………………………………………………………………………
11. Spleen……………………………………………………………………………………………………………..

Additional information e .g Physical defects or impairment, infections, chronic or family diseases (e.g. Sickle cell)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………..

I (full name) ……………………………………………………………………… Certify that, the above student is fit/is not fit to pursue Secondary Education.

Designation ……………………………………………………………………………

Station………………………………………….. Signature…………………………….

Date………………………………………………. Rubber Stamp ……………………………………………